BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kwanza – Tarehe 14 Februari, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. KIAPO CHA UAMINIFU:

**Mhe. Shariff Ali Shariff.**

## II. TAARIFA YA SPIKA:

## III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 09 Disemba, 2023.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Nam. 12 ya 2019 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar Kusimamia Huduma za Serikali Mtandao Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Nam. 12 ya 2019 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar Kusimamia Huduma za Serikali Mtandao Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

## IV. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

123. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tangu ukoloni ulipong'olewa hapa Zanzibar, wananchi wetu wamepata fursa pana ya kujiamulia mambo ya nchi yao pamoja na kujitawala.

Je, kwa kiasi gani dhana ya utawala bora imezidi kuimarika katika awamu ya Serikali ya sasa.

**Ofisi ya Kazi, Uchumu na Uwekezaji:**

75. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar alikuwa na nia njema na nchi hii kwa kujenga hoteli ya Bwawani ili kuweza kuongeza nguvu ya uwekezaji katika huduma ya Utalii Zanzibar. Hata hivyo, hivi sasa majengo hayo yamegeuka magofu.

(a) Je, nini hatma ya magofu hayo.

(b) Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya hatma ya hoteli ya Bwawani.

(c) Je, ni changamoto gani iliyopelekea hoteli hiyo kufikia hali iliyopo sasa kwa majengo hayo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

36. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Inasikitisha kwamba, katika eneo la Bububu Jeshini Meli Saba, kuna mtu amekodi eneo na kuweka *bar* iitwayo Machatu ambayo inatoa huduma katika eneo hilo. Hata hivyo, katika eneo hilo panapigwa mziki kwa sauti kubwa hadi zaidi ya saa 9 za usiku, jambo ambalo linawasumbua na kuwaudhi wenye hoteli zinazolaza wageni karibu na eneo hilo.

(a) Je, kuna sheria yoyote au ruhusa maalumu inayoruhusu upigaji mziki kwa sauti kubwa hadi zaidi ya saa 9 za usiku.

(b) Je, mziki unaopigwa zaidi katika siku za Alkhamis na Ijumaa katika *bar* hiyo ni baada ya kupatikana kibali maalumu au kwa kufuata Sheria.

(c) Je, ni hatua gani Serikali imechukua kupunguza tatizo hili baada ya kulalamikiwa mara nyingi hasa katika Ofisi za Serikali.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

155. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Ni sababu zipi zinazopelekea mradi wa ujenzi wa gofu la Bikhole kusuasua licha ya kuanza vyema kwa hatua za mwanzo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

94. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni kwa kiasi gani Sera ya Michezo inaakisi chachu ya kuwa na Utalii wa Michezo (Sport Tourism) hapa nchini mwetu.

95. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni utaratibu na mikakati gani ambayo Wizara yako inaiandaa katika kurejesha vugu vugu la michezo nchini.

**Wizara ya Afya:**

93. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizofanikiwa sana katika kutokomeza maradhi ya malaria duniani.

Je, kwa hivi sasa tathmini iko vipi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

32. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa muda mrefu sasa tumeshuhudia nchi za majirani zetu na duniani kwa ujumla kuwa wanawafundisha wananchi wao fani mbali mbali za stadi za maisha, ili kuwasaidia wananchi hao baada ya kuhitimu masomo yao.

(a) Je, Serikali yetu inatathmini vipi jambo hili kupitia mitaala inayotolewa nchini.

(b) Je, ni upi muitiko wa wanafunzi wetu kwenye skuli zetu za elimu mbadala na zile zinazotoa elimu inayolingana na stadi hizo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

29. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nane ni kuwasaidia wavuvi wetu kujikwamua na maisha, lakini hadi sasa dhamira hiyo bado haijafikiwa kwa sababu boti walizopewa wavuvi wetu hao hazijakidhi haja.

(a) Je, Serikali haioni kuwa boti walizopewa wavuvi wetu hazina uwezo wa kufika bahari kuu, ambako ndiko kwenye samaki wakubwa.

(b) Je, ni lini hasa wavuvi wetu watapatiwa boti za kisasa zinazoweza kuhimili mkondo ili kwenda kuvua bahari kuu kwenye samaki wakubwa.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

106. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kumekuwa na malalamiko ya wateja mbali mbali kuhusiana na tatizo la baadhi ya wafanyabiashara kupunguza mizani za vipimo mbali mbali vya biashara.

(a) Kwa kiasi gani Wizara yako inalifahamu jambo hili.

(b) Je, ni taratibu gani za kikanuni na kisheria zinazofuatwa kwa wafanyabiashara kama hao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

85. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na ukarabati uliofanywa katika kisima cha Kangani Sokoni ambapo tayari kishajengwa na kuanza kuwekewa miundombinu yake lakini bado pampu haijawekwa.

Je, ni lini pampu hiyo itawekwa katika kisima hicho ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

40. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kama inavyofahamika, Serikali iliingia mkataba na kampuni ya ufaransa (AGL) kuendesha bandari ya Malindi Zanzibar na Baraza la Wawakilishi lilielezwa na Serikali kwamba mwekezaji atawekeza kwenye vifaa (equipments) na utaalam (expertise) ili kuongeza ufanisi wa operesheni za bandari hasa katika kupunguza muda wa meli kukaa nangani kusubiri kupakuliwa mizigo.

(a) Je, ni utaalam (expertise) wa aina gani na wataalamu wangapi mpaka sasa wameajiriwa kwenye bandari hii na kwa kiasi gani ufanisi umeongezeka.

(b) Je, kwa wastani ni kiasi gani cha mapato kimepatikana na Serikali imepata kiasi gani cha mapato hayo.

(c) Je, ni wafanyakazi wangapi wa Bandari wameacha, wameachishwa au wamehamishwa kazi kutokana na ubinafsishwaji huo wa bandari.

52. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Imefahamika kwamba mara tu baada ya kupitishwa kwa Bajeti za Wizara na Serikali Kuu za mwaka 2023/2024, Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) ilihamishiwa kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwenda Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

(a) Je, kuna sababu zipi za kitaalamu zilizopelekea mabadiliko hayo.

(b) Je, ni mabadiliko yepi ya kiufanisi yamepatikana tokea ZBA ilipohamishiwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

(c) Je, Serikali haioni kwamba kuhamisha Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA), mwenye dhamana ya kusimamia na kushauri kuhusiana na majengo ya Serikali, na kuipeleka kwenye Wizara dhamana ya ujenzi kunaweza kusababisha mgongano wa kimaslahi na utata katika utendaji.

## V. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Nam. 12 ya 2019 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar Kusimamia Huduma za Serikali Mtandao Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**14 Februari, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**